# RSV

**Virusi vya upumuaji vya syncytial (RSV) ni virusi vya kawaida vya upumuaji ambavyo vinaweza kusababisha dalili kali na zinazohatarisha maisha kwa watoto wachanga na watu wazima wazee.**

**Chanjo za RSV zinapatikana kwa watu wazima wazee (50+), watoto wachanga, na wajawazito ili kusaidia kuwalinda wale walio katika hatari kubwa.**

## Ni nani yuko katika hatari?

- Watoto wachanga, haswa wale walio chini ya miezi 6
- Watoto wadogo waliozaliwa kabla ya wakati
- Watoto na watu wazima ambao tayari wako na matatizo mengine ya afya
- Watu wazima wazee
- Watu wenye kinga dhaifu
- Watu wazima wanaoishi katika vituo vya utunzaji wa muda mrefu

## Dalili ni zipi?

- Homa
- Kutoa Makamasi
- Kufungana
- Kukohoa
- Koo Linalouma
- Kukoloma
- Kuumwa na Kichwa
- Kuchoka

## Viruzi hivi hueneaje?

RSV inaenea kwa urahisi kupitia matone ya kupumua kutoka kwa kikohozi, kupiga chafya, au unapogusa sehemu zenye virusi na kisha kugusa uso wako.

**Changanua msimbo wa QR kwa maelezo zaidi.**

**Wasiliana na mtoa huduma wako wa afya ikiwa una wasiwasi au una maswali kuhusu dalili.**

## Punguza kuenea kwa RSV:

- Safisha sehemu zinazoguswa mara kwa mara
- Epuka kugusana kwa karibu na wagonjwa
- Kaa nyumbani unapokuwa mgonjwa
- Vaa barakoa ikiwa uko mgonjwa
- Osha mikono yako mara kwa mara
- Funika kikohozi chako na unapopiga chafya
- Pata chanjo ikiwa unastahiki



Department of Public Health
CITY OF PHILADELPHIA

Majira ya Baridi 2026

*Piga simu kwa 911 au nenda kwa ER MARA MOJA ikiwa wewe (au mtoto wako) mnapata shida ya kupumua, hunywi maji ya kutosha, au ikiwa dalili*

**RSV husambaa zaidi wakati wa miezi ya msimu wa vuli na wa baridi. Ikiwa uko katika hatari kubwa ya kuambukizwa RSV kali, au ikiwa unaingiliana na wale walio katika hatari kubwa sana ya kuugua RSV, unapaswa kuchukua tahadhari zaidi ili uendelee kuwa na afya njema.**

## Watu



Chanjo mpya za RSV zinaweza kukulinda kutokana na maambukizi makali ya RSV.

Dozi moja inapendekezwa kwa watu wazima wote wenye umri wa miaka 75 na zaidi.

Baadhi ya watu wazima wenye umri wa miaka 50 na zaidi wako katika hatari kubwa ya kupata ugonjwa mbaya wa RSV. Zungumza na mtoa huduma wako wa afya kuhusu ustahiki.

## Wajawazito

Wajawazito wanapaswa kupata chanjo ya RSV ili kuzuia magonjwa makali kwa watoto wao wachanga.

Zungumza na mtoa huduma wako wa afya kwa maelezo zaidi.



## Watoto Wachanga



Watoto wachanga walio chini ya miezi 8 ambao wazazi wao hawakupokea chanjo ya RSV wakati wa ujauzito wanapaswa kupokea kingamwili za RSV katika msimu wao wa kwanza wa RSV.

## Maswali Yanayopendekezwa ya Kumuuliza Daktari Wako

- Je, nina matatizo yoyote ya kiafya ambayo yanaweza kuniweka katika hatari kubwa ya RSV kali?
- Ni nini muhimu kwangu kujua kuhusu RSV na virusi vingine vya kupumua msimu huu?

Department of Public Health
CITY OF PHILADELPHIA

Programu ya Utayari wa Afya ya Umma | 215-683-0806

Kwa maelezo zaidi kuhusu RSV, zungumza na mtoa huduma wako wa msingi, au tembelea cdc.gov/rsv